**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu ……..**

**Mkuu wa Shule 0713281261**

**Makamu Mkuu wa Shule.0620108276**

**Shule ya Sekondari Mkindi,**

**S.L.P. 90,Kilindi.**

**Tarehe 13/6/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..................................................................**

**S.L.P ...........................…………………………………**
**…………………………………**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MKINDI HALMASHAURI YA KILINDI MKOA TANGA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024,na atasoma tahasusi ya HGK na HGFa

Shule ya Sekondari Mkindi ipo umbali wa Kilometa 18… Kaskazini/Kusini/Mashariki/Magharibi mwa Mji wa Handeni Usafiri wa basi kutoka mjini Handeni unapatikana katika kituo cha mabasi ya Handeni Nauli ni Shilingi 3000 shuka MSENTE na chukua pikipiki sh 5000 mpaka shuleni, na ukishuka handeni waweza kuja kwa pikipiki moja kwa moja mpaka shuleni kwa Shilingi 10000 kwa bajaji 15000 .

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/07/2024.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii kwa wasichana ni mshono wa sketi ni V isiyobana na isiwe fupi na wavulana suruali sio modo (kitambaa ni lucas *rangi ya bluu sio dark bluu kwa wote pea 2*). Kwa mzazi anayependa kununua shuleni zinapatikana shule kwa gharama ya 20,000 kwa moja hii ni kuepuka kuchanganya rangi.

ii. Mashati mawili mawili meupe ya mikono mirefu aje nayo kwa wanafunzi wa kiislamu watashona nusu kanzu nyeupe.

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi kwa wanafunzi wa kiislamu.

iv. Sare ya Michezo ni track suit za dark blue yenye nembo ya bendera ya Tanzania na mistari ya njano na bluu pembeni kwa wote.

v. Aje na jezi ya Tanzania ya bluu kwa wote kwaajili ya michezo.

vi. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi au juma na roza kwa wasichana.

vii. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu kwa wasichana na soksi za kijivu kwa wavulana.

viii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

ix. Aje na Sweta rangi ya kijivu iliyoiva (dark gray) kwa wote

(ii)

i. Nguo za kushindia gauni 1shamba dress rangi ya kaki iliyoiva kitambaa cha ESTEM namba moja mshono wa dera refu mpaka chini na sketi 1 ya kaki iliyoiva mshono wa solo kwa wasichana na suruali isiyo bana rangi ya kaki iliyoiva kitambaa cha ESTEM namba moja na tshirt ya kushindia yenye nembo ya shule zinapatikana maduka yaliyo karibu na shule kwa sh 13,000/=

ii. Tai 1 ya bluu ya kati yenye michirizi meupe.

x. Tisheti 1 kwaajili ya darasani yenye nembo ya shule inapatikana shule kwa sh 13000/= kwa wote. Zinapatikana shule

iii.Aje na bima ya afya .

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 8 counter book quire 3,na madogo 7 ya mazoezi

ii. **Ream (A4)** aina ya mondi na 1 au GSM ya Karatasi aje nazo Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Non programmable Calculator;
v. Godoro futi 2 na nusu.
vi. Mashuka Jozi 2 ya pink kwa wasichana,na shuka 2 za bluu kwa wavulana ,blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1cheupe wasichana na dark bluu wavulana .
vii. Nguo za ndani za kutosha;na singlend nyeupe na blazia nyeupe
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko,chupa ndogo ya chai na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja 1, jembe 1, fagio 1 wa chelewa usio na mti kwa wote na soft bloom na reki kwa wasichana na rubber squizer na panga kwa wavulana.
xi. Aje na tochi au taa ya solar kwa tahadhari umeme ukukatika.
xii. Aje na Nakala ya cheti cha kuzaliwa na Result slip ya f4.
xiii. Kila mwanafunzi aandike jina Lake kwenye sare zake na vifaa vyake.
xiv. Aje na Tranka na kufuli zake.
xv. Aje na malapa ya kuogea.

ORODHA YA VITABU;

i). History -History for secondary school form 5&6 by TIE

- Essential History for secondary school paper1&2 by SalehYasin

ii). Kiswahili -Sarufi kidato cha 5&6 cha TIE

-Nadharia ya Kiswahili kidato cha 5&6 cha Nyambali Nyangwine au TIE

iii). Geography- A Comprehensive Approach to physical Geography by DT Msabila

- Practical Geography; map reading photography Advance level 5&6

iv). General studies For Advance level by Joannes

v).Kamusi ya kiswahili sanifu. (vi)Fasihi ya kiswahili sanifu cha TIE

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

ilipwe kwenyewe namba ya akaunti **NMB 42610000565** na aje na benk pay slip

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

3. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.p

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni**

**ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Kama hujaelewa tafadhali piga simu kwa Namba zilizopo.

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MKINDI HIGH SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS**

MKINDI SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 90,
**SONGE – KILINDI**

Date......................

**MEDICAL OFFICER, GOVERNMENT HOSPITAL**

.......................................................
NAME OF STUDENT.................................................
Please examine the above named student to ascertain his fitness for admission to pursue studies.

................................................
**Head Mistress/Headmaster**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin...................................................................................................................
Eyes...................................................................................................................
Ears...................................................................................................................Chest........................
.........................................................................................
Spleen...............................................................................................................
Abdomen..........................................................................................................
Urine.................................................................................................................
Stool...................................................................................................................Hemoglobin(Hb)........
.........................................................................................
I consider that:

- He is of good health, free from infectious diseases, worms, bilharzias and fit to pursue studies
- He is now fit to return to school after having been treated for................

..................................................**Name and Designation** **Signature**

**…………………………..** **……………………….**
**Official StampDate**

## UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MKINDI

**SEHEMU A:** (Ijazwe na Mwanafunzi)

Mimi (jina kamili)....................................................................................

Tarehe ya kuzaliwa...................................................................................

Dini...........................................................................................................

Kijiji.............................. Wilaya................................ Mkoa..........................

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia Kidatocha Tano Shule ya Sekondari Mkindi. Nathibitisha kuwa Nitatii na kufuata sheria zote za Shule kama zilivyo ainishwa. Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiriki katika Migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa Shule ili matatizo yatafutiwe ufumbuzi pindi yanapotokea.

Saini.............................................. Tarehe...........................................

**SEHEMU B:** (Ijazwe na Mzazi)

Mimi (Jina kamili) ..................................................Namba ya simu.........................

KIjiji.................................... Wilaya............................. Mkoa................................

Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mwanangu Nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya Shule. Nitahakikisha mtoto anaenda shule muda uliopangwa na nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na Shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.

Saini ya Mzazi ...........................................Tarehe.......................................

Jina la Mtendaji wa Kijiji..................................................................................

Saini................................. Tarehe............................. Mhuri..........................

Jina la Mtendaji Kata.................................................................................

Saini................................. Tarehe.............................Mhuri………………………

**PICHA NA NAMBA ZA SIMU ZA WAZAZI/WALEZI NA NDUGU WATAKAOWASILIANA AU KUFIKA KUMTEMBELEA AWAPO SHULENI**

1.Picha

Jina(Matatu)

__________________________________________

Uhusiano na mwanafunzi ________________________

Namba za simu ______________________________

2.Picha

Jina (matatu)

____________________________________

Uhusiano na mwanafunzi ____________

Namba za simu ____________________

3. Picha

Jina(matatu)

____________________________________

Uhusiano _____________________

Namba za simu ____________________________

4. Picha

Jina(matatu)

________________________________

Uhusiano __________________

Namba za simu _________________

**NB: Hatarusiwa mtu mwingine yoyote kumtembelea au kufanya nae mawasiliano akiwa hapa shuleni.**

**ANGALIZO**

Hakikisha unafika Shuleni ndani ya wiki ya kwanza ya kufungua shule na mwisho wa kuripoti ni wiki mbili kuanzia tarehe ya kufungua Shule na baada ya hapo nafasi yako atapewa mtu mwingine endapo utakuwa hujafika Shuleni.

**KAULI MBIU YETU; "MKINDI BILA DARAJA LA PILI HAKIKA INAWEZEKANA"**

KARIBUNI SANA MKINDI SEKONDARI

**CHUKI A. ATHUMANI**
**MKUU WA SHULE**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0713281261**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0620108276**